

Aprili 28, 2021

Sasisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu ya Kaunti ya Fayette

Ndugu Jumuii ya FCPS,

Utafutaji wa kuchagua msimamizi mpya unaathiri jamii yetu yote. Kwa hivyo tumejitolea kukujulisha kuhusu maendeleo yetu. Nimefurahia kushiriki kwamba utaftaji unabaki kwenye ratiba. Katika awamu hii inayofuata, kamati ya uchunguzi itajifunza zaidi juu ya waombaji:

- Ijumaa [siku ya tano] iliyopita, kamati ya uchunguzi ([screening committee](#)) ilitumia siku hiyo kukagua hati za waombaji. Hii ilijumuisha wasifu, maelezo binafsi (CVs), barua za fafanuzi, na orodha za udhamini za mwanzo
- Kamati ya uchunguzi ikawachagua waombaji ambao walitimiza sifa za chini na wakalingana kwa karibu na ustadi wa kitaalam na uwezo wa kibinafsi ulioainishwa katika Profaili ya Msimamizi ([Superintendent Position Profile](#)). Kamati inafurahi kujifunza zaidi juu ya wagombea hawa kupitia duru ya kwanza ya mahojiano.

Baada ya duru ya kwanza ya mahojiano, Greenwood / Asher and Associates watakamilisha ukaguzi wa udhamini. Wajumbe wengine wa kamati ya uchunguzi wanaweza pia kujitolea kushiriki katika mchakato wa utaftaji. Wito wa udhamini zimetolewa kwa wasimamizi, wenzao, na wowote wale ambao wamefanya kazi kwa karibu na wagombea na wanaweza kushuhudia ustadi wa uongozi na mafanikio ya wagombea. Habari iliyokusanywa kupitia awamu hii ya utaftaji itashirikiwa na kamati ya uchunguzi.

Ningependa kutoa tena shukrani zangu kwa kamati ya uchunguzi. Nina hakika kila mtu ana hamu kubwa kama mimi kujifunza zaidi juu ya wagombea, lakini awamu hii inachukua muda mwingi na kuzingatia sana, na hivyo kuweka kamati ikilenga katikati ya Mei. Tunatambua kuajiriwa kwa msimamizi ni uamuzi muhimu zaidi ambao bodi ya shule inaweza kufanya na tutaendelea kukusasisha juu ya mchakato. Kwa ratiba kamili ya matukio, tafadhali tembelea <https://www.fcps.net/search>.

Kwa dhati,

Tyler Murphy
Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu ya Kaunti ya Fayette